Njia Inayoelekea Emau

(The Road To Emmaus)

Na

Terry Warford

Njia Inayoelekea Emau
(The Road To Emmaus)

na

Terry Warford

Novemba 12, 2011

Njia Inayoelekea Emau

Luka 24 inashiriki hadithi ya kweli ya Yesu kufufuliwa katika wafu. Inaongeleaa makundi kadhaa waliomwona alipofufuka.

Moja kati ya haya lilikuwa ni kundi la wanaafunzi wawili waliokuwa wakitembeaa kutoka Yerusalemu hadi katika kijiji kilichoitwa Emau. Hadithi hii imeandikwa katika mistari ya 13-35 ya kitabu cha Luka, na inasema jinsi Yesu alivyoungana nao katika matembezi hayo na kuongea. Ilipofika jioni, walimwalika alale pamoja nao na kupumzika, na hatimaye waligundua kwamba ni Yesu katika kuumega mkate.

Hadithi hii inaipendezesha picha nzuri ya uhusiano amabo tunaweza kuwa nao na Yesu Kristo leo, na Baba yetu aliye mbinguni kupitia Yesu. Na yote ilifanywa iwezekane kwa kifo cha Kristo, maziko na ufufuo.

Katika dhana halisi tunaweza kutembea na Yesu leo, tujifunze naye, na kumega mkate pamoja naye kama walivyofanya katika njia ya Emau.

Tunaweza kutembea na Yesu katika hali ya ushirika, na kufanya kama alivyofanya. Tunaweza kujifunza na Yesu unabii huu uu ulitimizwa siku ile, na pia kuyaona maandiko ya Agano Jipya kama yalivyotolewa na Yesu. Na tunaweza kumega mkate na Yesu kwa kuonyeshaa shukrani zetu kwa chaakula na baraka anazotupatia, na kwa njia ya kipekee katika ushirika wa meza ya Bwana.

Kutembea Na Yesu

Hebu tuangalie kwanza katika kutembea na Yesu. Luka 24:13-15, "*Na tazama siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili. Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yaliyotukia. Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.*"

Tunaweza kutembeaa na Yesu leo pia, ambacho namanisha ni kwamba tunaweza kuwa na ushirika naye, na kutembea katika mwelekeo kama wake na katika hatima ileile. Hii ni baraka tuliyopewa katika wakati wa Kristo, sasa amefufuka kutoka katika wafu. Fikiria kuhusu nyimbo nyingi zinazoonyesha ukweli huu. "Alama za unyayo wa Yesu", "Natembea na Mfalme", na "Kukanyaga Katika Nuru" tukitaja chache.

Tuna ushirika na Yesu kwa njia nyingi. Awali ya yote kuna ushirika na Yesu kupitia neno lake, 1 Yoh. 1:3, "*Hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi na ushirika*

wetu ni pamoja na Bwana na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo." Je waona? Mitume na waandishi wengine wa zamani walimwona Yesu. Walihubiri na kuandika neno la Mungu, kama Yesu mwenyewe alivyowapa. Kupitia neno lao tunaweza kuwa na ushirika pamoja nao, na Yesu aliyewapa.

Katika Mat. 18:20 tuanaona kwamba tuna kuwa na ushirika na Yesu tunapokuwa na ushirika na wengine. "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao*." Tuna ushirika pamoja naye kupitia imani, Efe. 3:17, "*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shinaa na msingi katika upendo;*" Tuna ushirika naye kupitia utii, Yoh. 14:23, "*Yesu akajibu akamwambia, mtu akinipenda atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake*." Tuna ushirika na Yesu tunapoteseka pamoja naye, Fil. 3:10, "*Ili nimjue yeye na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifanananishwa na kufa kwake;*"

Maandiko haya yanaonyesha kwamba kutembea na Yesu ni ushirika, ni lazima tutembee katika mwelekeo uo huo. Amosi 3:3, "*Je watu wawili waweza kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana*?" Hakuwezi kukawa na ushirika, hakuwezi kuwa na kutembea na Yesu kama tukisisitiza kwenda katika njia yetu wenyewe, kama tunavyosoma katika 1 Yoh. 1:5-7, "*Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu ya kwamba Mungu ni ruhu wala giza lo lote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli; bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu Mwana wake yatusafisha dhambi yote.*"

Alafu inafuata kwamba tukienda katika mwelekeo huo kama Yesu, tunatarajia kufika katika makazi yayo hayo. Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi*." Ms ya 2-3, "*Nyumabi mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*" Ni ahadi nzuri iliyoje!

Kujifunza Na Yesu

Kama mitume wengine wawili walivyokuwa wakitembea na Yesu, kabla hata hawajatambua kuwa alikuwa yeye, walikuwa wakiongea kuhusu tukio la karibuni. Walikuwa wakijadili jinsi Yesu alivyosulubiwa, na hawakuielewa, kwa sababu walitarajia vitu tofauti. Katika ms ya 25-27 ya Luka 24 Yesu anaanza kujifunza nao na kuwafunulia unabii mwingi aliyotimiza, "*Akawaambia enyi msiofahamu,*

wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?akaanza kutoka Musa na manabii wote akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe."

Tunaweza kujifunza na Yesu pia, katika hali ambayo tunaweza kujifunza unabii huu uu, na kuona kwamba Yesu alizitimiza, na akaitangaza duniani. Tunaweza kuona zaidi kwamba Yesu anatoa maandiko ya Agano Jipya kwa dunia, kupitia mitume wake.

Yesu alitangaza mara nyingi kwamba maneno aliyokuwa anatoa yalitoka kwa Mungu. Tukiangalia mfano mmoja, tafadhali fungua Yohana 12:49-50, ambapo Yesu alisema, "*Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo*."

Yesu alitoa neno la Mungu katika ulimwengu kupitia mitume wake, tena tunaweza kuona katika maandiko mengi. Ebu tuangalie katika Yohana 17:6-8, ambapo Yesu alisema, katika kumwomba Mungu, "*Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako ukanipa mimi na neno lako wamelishika. Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako. Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma*." Sio tu kwamba mitume walihubiri hili neno, lakini pia waliliandika, ili kwamba tuwe nayo leo, 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana*."

Kumega Mkate Na Yesu

Katika mwendelezo wa hadithi tunawaona mitume wawili wakimega mkate pamoja na Yesu katika Luka 24:28-31, "*Wakakaribia kile kijiji walichokuwa wakienda naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. Wakamshawishi wakisema, kaa pamoja nasi kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao. Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate akaubariki akaumega, akawapa. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua kisha akatoweka mbele yao*."

Ebu tuangalie njia mbili ambazo tunaweza kumega mkate na Yesu leo.

Kwanza kabisa, ebu tuelewe kwamba tunamega mkate pamoja naye kwa njiaa ya kiroho tunapoonyesha shukurani zetu kwa Mungu kupitia Yesu kwa chakula na baraka zingine alizotupatia. Hakika ni mfumo wa

hatua tatu: kukubali baraka zake, tuzishukuru, na kuonyesha shukurani zetu kwake.

Katika Fil. 4:19 tunaona mtume Paulo anashukuru utoaji wa Mungu kwetu kupitia Yesu, "*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.*" Katika 1 Tim. 4:4-5 tunaona hatua zingine mbili, kuwa mwenye shukurani na kuionyesha katika sala, "*Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukurani; kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.*"

Ya pili, ambayo ni maalum sana, tunavyo mega mkate na Yesu ni katika huduma ya ushirika. 1 Kor. 10:16, "*Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo?*" Tunafanya hivyo katika kumbukumbu ya shukurani ya jinsi Yesu alivyoutoa uhai wake katika msalabaa wa Kalvari kwa niaba yetu, 1 Kor. 11:23-26, "*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, aksema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana ahata ajapo.*"

Hivyo tunaona kwamba hadithii hakikaa inatupendezeshea taswira ya uhusiano ambao kila mmoja anaweza kuwa nao na Yesu kama Wakristo. Ushirika wetu na yeye kiroho badala ya kimwili, lakini inamaan inayofanana.

Tunaweza kutembea na Yesu, katika hali ya ushirika, na kwenda katika uelekeo unaofanana. Tunaweza kujifunza na Yesu, katika hali ya kuona unabii alioutimiza, naa kujifunza maandiko ya Agano Jipya aliyotoa. Naa tunaweza kumega mkate pamoja naye, tunapoonyesha shukurani zetu kwa Mungu kupitia Yesu kwa ajili ya chakula aliotupatia, na tunapokumbuka katika ushirika wa meza ya Bwana dhabihu yaa Kristo ya upendo kwetu msalabani.

Ebu tufunge naa Wag. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Katika upendo wa Kristo,

Ndg. Terry Warford